



# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## TANGAZO LA MAEneo YA KUPANGISHA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na. ENEO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA	
1.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Steshenari
2.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Steshenari
3.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Saluni ya Kike
4.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Saluni ya Kiume
5.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Huduma ya kushona nguo
6.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Huduma ya Wakala wa Kifedha (Mitandao yote)
7.	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Hosteli ya Dkt. J. P. J Magufuli (Business Park)	Duka la michezo ya Play Station na Duka la kuuza filamu (Play station and movie shop)

Kwa tangazo hili, UDSM inawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma hizo. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 228 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi Elfu Kumi Tu (**TZS 10,000/=**) kupitia ‘Namba ya Kumbukumbu’ ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **05 Disemba 2023** itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi waombaji wote wanatakiwa kuwepo katika Hosteli za Dkt. J. P. J Magufuli Business Park.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo ya maombi yao kwa njia ya barua.

### IMETOLEWA NA

**NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA**

**27.11.2023**